



Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam (UWABA)
SLP 12247
Dar es Salaam

www.geocities.com/uwabadar
email: uwabadar@yahoo.co.uk
0713 652642 / 0754 568512

11 Aprili 2007

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam
Dar es Salaam

Meya wa Manispaa ya Ilala
Dar es Salaam

Meya wa Jiji la Dar es Salaam
Dar es Salaam

Mkurugenzi
Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam
Dar es Salaam

Mkurugenzi
Halmashauri ya Manispaa ya Ilala
Dar es Salaam

SUMATRA
Dar es Salaam

YAH: SERA YA KUPIGA MARUFUKU MAGUTA MJINI NA KARIAKOO

Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam ni NGO ambayo imesajiliwa na serikali. Malengo yetu ni kuhamasisha baisikeli kama usafiri wa jiji na kulinda haki za wapanda baisikeli. Unaweza kupata taarifa zaidi kwenye tovuti yetu www.geocities.com/UwabaDar.

Baisikeli zina faida nyingi kama usafiri wa jiji. Haziharibu mazingira, zinapunguza msongamano, ni usafiri wa bei nafuu na zinapunguza umasikini. Pia, maguta yanasaidia ajira na kuwapatia riziki wananchi wengi. Maguta yanasafirisha bidhaa za aina mbali mbali mjini na yanajenga uchumi. Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ina sera ya kuhamasisha wapanda baisikeli katika mradi wao wa DART.

Kwa hiyo tumeshangazwa sana na tangazo la juzi juzi la Manispaa ya Ilala kupiga marufuku maguta mjini na Kariakoo. Sababu iliyotolewa ni kwamba maguta yanasababisha msongamano. Hii sababu imetushangazwa sana kwa sababu msongamano unasababishwa zaidi na magari binafsi. Kuna barabara nyingi mjini ambazo zina msongamano bila guta hata moja.

Hata kama maguta yataondolewa, bado maduka na masoko yatahitaji bidhaa. Kwa hiyo magari zaidi yatatakiwa kusafirishia bidhaa, msongamano utaongezeka zaidi na mazingira yataharibika zaidi. Aidha, kwa sababu magari yanatumia mafuta, kila mara mafuta yanapanda bei, bidhaa zinapanda bei vile vile. Sehemu kama Kariakoo hakuna nafasi ya malori makubwa, kwa hiyo maguta yanafaa sana kutoa huduma hizi muhimu.

Mwalimu Nyerere aliunga mkono wapanda baisikeli tangu uhuru. Sera za serikali kama MKUKUTA zinasema serikali inajaribu kuondoa umasikini. Sera ya kupiga marufuku maguta hailingani na MKUKUTA kwa sababu inaongeza umasikini wa wananchi wanaofanya biashara za maguta. Pia, uamuzi wa kupiga marufuku maguta umefanywa bila kutafuta mawazo ya wananchi.

Kwa ujumla tunaona sera hii ni uonevu kwa wananchi. Tunaomba Manispaa ya Ilala isiendelee na sera hii. Aidha, tunaomba Manispaa ya Ilala ihamasishe wapanda baisikeli wote, na ijenge sehemu za barabara hasa kwa baisikeli, maguta, mikokoteni na watembea kwa miguu.

Tunashukuru kwamba maombi yetu yatafikiriwa.

Wako katika ujenzi wa Taifa,

Fredrick “Mejah” Mbuya,
Mwenyekiti UWABA